

TAARIFA YA TATHMINI YA MATOKEO YA MTIHANI/UPIMAJI MWAKA 2024

Utangulizi

Baraza la Mitihani la Tanzania limetangaza matokeo ya mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) 2024, Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) 2024, Mtihani wa Kidato cha Sita (ACSEE) 2024, Upimaji wa Kitaifa Darasa la Nne (FTNA) 2024 na Kidato cha Pili (FTNA) 2024.

Hali ya Ufaulu

Tathmini ya ufaulu inaonesha kupanda kwa ufaulu katika Mtihani wa Kidato cha Sita, Kidato cha Nne, Upimaji wa Kitaifa Darasa la Nne na Kidato cha Pili. Aidha, tathmini hiyo imeonesha kushuka kwa ufaulu katika mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2024.

Hali ya ufaulu katika mitihani/upimaji mwaka 2024 ni kama ifuatavyo;

- a) Katika Mtihani wa Kidato cha Sita (ACSEE) 2024 jumla ya wanafunzi **5,860** kati ya **5,862** sawa na asilimia **99.97** wakiwemo wavulana **3,473** na wasichana **2,387** wamefaulu mtihani huo. Mkoa umepata GPA ya **2.51**. Tathmini inaonesha kuwa ufaulu umepanda kwa GPA ya **0.9** ukilinganisha na ufaulu wa mwaka 2023 ambao ulikuwa ni GPA ya **2.60**.
- b) Katika Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) 2024 jumla ya wanafunzi **19,931** kati ya **22,104** sawa na asilimia **90.17** wakiwemo wavulana **9,068** na wasichana **10,863** wamefaulu mtihani huo. Mkoa umepata GPA ya **3.4229**. Tathmini inaonesha kuwa ufaulu umepanda kwa GPA ya **0.18** ukilinganisha na ufaulu wa mwaka 2023 ambao ulikuwa ni GPA ya **3.60**.
- c) Katika Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (FTNA) 2024 jumla ya wanafunzi **31,010** kati ya **37,299** sawa na asilimia **83.14** wakiwemo wavulana **13,867** na wasichana **17,143** wamefaulu mtihani huo. Mkoa umepata GPA ya **3.5490**. Tathmini inaonesha kuwa ufaulu umepanda kwa GPA ya **0.16** ukilinganisha na ufaulu wa mwaka 2023 ambao ulikuwa ni GPA ya **3.70**.
- d) Katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) jumla ya wanafunzi **53,158** kati ya **59,690** wakiwemo wavulana **25,616** na wasichana **27,542** walifaulu mtihani huo. Mkoa umepata ufaulu wa asilimia **89.06**. Tathmini inaonesha kuwa ufaulu umepanda kwa asilimia **0.14** ukilinganisha na ufaulu wa mwaka 2023 ambao ulikuwa asilimia **88.92**.
- e) Katika mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) jumla ya wanafunzi **38,274** kati ya **45,761** wakiwemo wavulana **17,866** na wasichana **20,408** walifaulu mtihani huo. Mkoa umepata ufaulu wa asilimia **83.64**. Tathmini inaonesha kuwa ufaulu umeshuka kwa **0.08** ukilinganisha na ufaulu wa mwaka 2023 ambao ulikuwa ni asilimia **83.72**.

Mikakati ya Kuinua Ufaulu

Mkoa umepanga mikakati ya kuhakikisha ufaulu katika mitihani/ufaulu unapanda. Mikakati hiyo ni kama ifuatavyo;

- i. Shule kuwatumia Walimu wa kujitolea ili kukabiliana na uhaba wa Walimu.
- ii. Kuimarisha ushirikiano wa walimu na wazazi katika shughuli za maendeleo ya shule.
- iii. Kutumia MEWEKA na Jumuhiya za ujifunzaji katika kuwajengea uwezo walimu ili waweze kuwa mahiri.
- iv. Halmashauri kuendelea kutenga bajeti kupitia mapato ya ndani pamoja na kushirikisha wananchi na wadau mbalimbali ili kujenga miundombinu ya shule kulingana na mahitaji;
- v. Kusimamia utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya shule ili iweze kukamilika kwa wakati na kutumika ili kuleta tija.
- vi. Kusimamia utekelezaji wa Elimu ya Kujitegemea kwa kuhakikisha shule zote kuwa na mashamba, bustani pamoja na ufugaji.
- vii. Kuimarisha ufuatiliaji wa mara kwa mara katika shule na kutatua changamoto za walimu ili kuweka mazingira bora ya ufundishaji na ujifunzaji.
- viii. Kuhamasisha jamii kuchangia chakula ili wanafunzi kupata lishe wakiwa shule.
- ix. Kuhakikisha kuwa Maafisa Elimu Kata na Walimu Wakuu wanaimarisha na kusimamia ufundishaji na ujifunzaji katika ngazi ya shule kwa kuhakikisha uwepo wa maandalizi ya ufundishaji kwa walimu yaani maazimio ya kazi, maandalio ya somo, zana za kufundishia na kujifunzia na nukuu za somo kwa kila mwalimu kabla na wakati wa kufundisha.
- x. Kushirikiana na mamlaka za serikali za vijiji na Kata katika kushughulikia masuala ya utoro wa wanafunzi ili kuimarisha mahudhurio yao shuleni.

Hitimisho

Mkoa kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa utasimamia na kuhakikisha kuwa mikakati iliyowekwa inatekelezwa ipasavyo ili kufikia malengo ya kupandisha ufaulu na kufikia ufaulu uliobora katika Mitihani/Upimaji mwaka 2025.